# MUNGU WANGU MBONA UMENIACHA

Na: Thohoma
@Nyamongo TRM Mara
20 March 2020
+255 675 886 608




1. *Watu wanionao hunicheka sana, hunifyonya wakitikisa vichwa vyao/ husema, amtegemee Bwana na amwokoe sasa ; apendezwa naye.*

2. *Kwa maana mbwa wamenizunguka, kusanyiko la waovu wamenisonga/ yamenizua mikono na miguu, naweza kuihesabu mifupa yangu yote.*

3. *Wanagawana nguo zangu, na vazi langu wanalipigia kura/ nawe Bwana usiwe mbali, Ee Mungu wangu, fanya haraka kunisaidia.*

4. *Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, katikati ya kusanyiko nitakusifu/ ninyi mnaomcha Bwana, msifuni enyi nyote, mlio wazao wa Yakobo mtukuzeni.*